**Learning by Ear**

**People Who Make a Difference**

# Kenya: Slum TV

**Author: Josephat Charo, DW Kisuaheli**
**Editor: Daniel Pelz/ Stefanie Duckstein**
EDITOR: Tony Dunham
Sound clips in DALET: Learning by Ear: **LbE_PEO_ Kenya Slum-TV**

---------------------------------------------------------------------------------------------

**Characters:**

**1 Narrator: Female voice**

**4 VOs:**

- **Collins Omondi, male, 21 years old**
- **Ephantus Kamau, male, early twenties**
- **Billian Okoth, male, in his twenties**
- **Esther Waweru, female, 21 years old**

---

**Introduction (Announcer):**

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga maisha yako kwa jina ”Watu wanaoleta mabadiliko. Leo hii tunambulisha kijana shujaa wa Kiafrika anayetumia kamera yake kuwaunganisha watu kutoka makabila mbalimbali ili waishi pamoja kwa amani nchini Kenya. Kijana huyo anaishi katika mtaa wa mabanda wa Mathare. Hilo ni eneo kubwa kabisa la mabanda nchini Kenya, liko katika mji mkuu, Nairobi.

**TEXT:**

**1. SFX Door opens**

**2. Soundbyte Collins Omondi 1 (English)**

*"Jina langu ni Collins Omondi, mimi ni mwananchama wa televisheni ya eneo ya mabanda la Mathare ( Slum TV). Ninatoka Mathare na nilizaliwa hapa jijini Nairobi. Nilianza masomo katika shule ya msingi ya Pumwani na baadaye nikahamia shule ya James Gichuru huko Dandora, ambako nilimaliza masomo yangu ya msingi. Sikuweza kuendelea na masomo yangu, mwaka 2002 mama yangu alifariki dunia. Kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mlezi wa familia yetu, haikuwezekana mimi kuendelea na masomo. Baba yangu anatokea Kisumu na dada yangu anaishi Kasarani hapa Nairobi. "*

**3. SFX Office Slum TV**

**4. Narrator**

Collins Omondi kijana wa miaka 21 anafanya kazi ya kujitolea katika mradi wa televisheni ya mtaa wa mabanda wa Mathare iitwayo Slum TV. Takriban watu laki saba wanaishi katika eneo hili lenye msongamano wa mabanda linalozungukwa na mabomba ya maji taka yaliyopasuka na kuzungukwa pia na mirundo ya takataka. Katika mwaka 2006 wanachama wa "Slum TV" walianzisha mradi wa kupiga filamu zinazoonyesha maisha halisi ya kila siku katika eneo hilo duni la mabanda na filamu hizo zinaonyeshwa kwa jamii. Mradi huu mkubwa unahusu "Kubadilishana Amani" vijana hao hutayarisha filamu zinanazolenga juhudi zinazofanywa na watu binafsi, vikundi au makanisa kuleta utulivu na kuendeleza amani baina ya watu wa makabila mbalimbali wanaoishi katika eneo hilo la Mathare. Slum TV pia huwaonyesha watu "Maalum" yaani watu ambao wamefanya mambo

yanayostahili sifa kama vile dereva bora, mnoaji visu hodari na hata mchezaji bora wa mpira wa miguu katika eneo hilo la mabanda. Collins alijiunga na Slum TV mwaka mmoja uliopita.

**5. Soundbyte Collins Omondi 2 (English)**

*"Rafiki yangu ndiye alienitambulisha kwenye Slum TV katika eneo hili la mabanda, kabla ya hapo nilikuwa katika shirika moja linaloitwa MYSA. (Inatamkwa MAISA) Nilikuwa mpiga picha, niliacha na nikaanza kutafuta njia zingine za kupata fedha ndipo rafiki yangu aliponiambia nijiunge na hii Slum TV. Nilikubali. Nikaanza kuja tangu wakati huo hadi hii leo. "*

**6. Narrator**

Collins alijiunga na Slum TV, kwa sababu anapenda kuwasaidia watu. Tangu alipoanza kufanya kazi hapa milango ya fursa mpya imeanza pia kufunguka. Ni hapa ndipo alipojifunza kutumia kamera na kutayarisha filamu, ujuzi ambao anautumia mahala pengine kurekodi na kutengeneza kanda za siku za kuzaliwa au harusi na anajipatia kipato kinacho msaidia kuendeleza maisha yake.

**7. SFX Sound of a door, a car**

**8. Narrator**

Collins Omondi anatupeleka nyumbani kwake huko eneo la mabanda la Mathare. Chumba chake ni kidogo na kimejengwa kwa mabati. Taa ya mafuta ni muhimu kwa sababu hata mchana kuna giza chumbani na huwezi kuona chochote bila kuwasha taa hiyo ya mafuta. Sakafu ya chumba hicho haina sementi, ni ya udongo. Ana vitu vichache tu ndani ya chumba chake, ijapokuwa ana kila kitu anachohitaji .

**9. Soundbyte Collins Omondi 3 (English)**

*“Hapa ndipo ninapotayarisha kiamsha kinywa changu, chakula cha mchana na pia chakula cha jioni. Hivi ni baadhi ya vyombo vyangu vya plastiki ambavyo huvitumia kuchotea maji. Hii ni stovu, ninatumia mafuta ya taa, huwa nanunua dukani. Hapa naweka vyombo vyangu na hivi ni vijiko. Hapa ndipo mimi huweka chumvi, majani ya chai na humu ni mwa kuwekea chai. Kwa kawaida mimi huweka chai humu ndani ya jagi la plastiki. Na hapa ndio naweka sabuni baada ya kuosha vyombo vyangu. Chupa hii ni ya kununulia mafuta ya taa ambayo huyaweka iwapo nitayahitaji kwa dharura. “*

**10. Narrator**

Kutoka Jumatatu hadi Ijumaa yeye huenda katika ofisi za Slum TV zilizopo katika mtaa jirani wa Eastleigh. Ingechukua dakika 15 kwa usafiri wa kawaida. Lakini mara nyingi hutumia zaidi ya dakika 45 barabarani hadi kufika safari yake, kwa sababu barabara za Nairobi huwa na msongamano mkubwa kila mara. Mbali na kuwa yeye ni mpiga picha, Collins amepewa pia jukumu la kuwa msimamizi wa shughuli za ofisi kwa sababu ya sifa ya uongozi aliyonayo. Na hii ina maana kazi zaidi katika majukumu yake ya kila siku. Lakini anasema kuwa haoni kama anashurutishwa kubeba majukumu zaidi.

**11. Soundbyte Collins Omondi 4 (English)**

*“Hapana! Sishurutishwi wala sisukumwi . Ni swala la kuwajibika, ninafurahia. Ninataka kuwaonyesha watu wa Mathare jinsi maisha yanavyokwenda na kuwatia moyo wajiunge na Slum TV. Kama kuna mtu anaweza kuchukua kamera na kwenda kufanya vipindi maalum. Hiyo itakuwa vizuri sana.”*

**12. SFX Editing ambience**

**13. Narrator**

Ofisini, wafanyakazi wenzake wanaendelea kutayarisha filamu. Slum TV ina wanachama 20. Vyumba vidogo viwili ndio mahala pao pa kufanyia kazi katika jumba moja la biashara. Kompyuta ya kupakata yaani laptop, kamera na rafu ya mbao iliyojaa kaseti za video zilizorekodiwa hapo awali, ndio vitu vilivyojaza vyumba hivyo viwili, hakuna nafasi tena iliyobakia. Esther Waweru, msichana wa miaka 21- mzaliwa wa mtaa wa mabanda wa Mathare, ni mmoja kati ya watu walioko leo hii. Collins ndie aliyempa moyo wa kujiunga nao.

**14. Soundbyte Esther Waweru 1 (English)**

*"Bila shaka, naipenda Slum TV. Haya ni maisha yangu, ni kila kitu changu. Slum TV ni Esther na Esther ni Slum TV. Siku ya kwanza nilipojiunga na Slum TV nilikuja na bahati kwa sababu nilikuta warsha kuhusu matumizi ya kamera inafanyika, nilijisemea waaa! Hiyo ni fani yangu. Nilitaka kujiunga na warsha hiyo! Binafsi, naona nuru katika maisha yangu ya usoni na kuhusu jamii nafikiri ingekuwa bora kama ingekuwa na chombo chake cha habari."*

**15. Narrator**

Maisha ya msichana huyu mwenye ari ya maendeleo yamebadilika kutokana na bidii ya Collins Omondi. Slum TV inawapa fursa ya kuondokana na umasikini. Ijapokuwa hawalipwi chochote kwa kazi wanayofanya, lakini wanaruhusiwa kutumia ujuzi wanaopata kujitafutia fedha kwa mfano kupiga picha za video katika maharusi, sherehe za siku za kuzaliwa au hata katika misiba na baadae kutengeneza kanda. Slum

TV haina kituo chake binafsi cha matangazo, lakini wahusika wanatarajia kuwa siku moja watafanikiwa kuanzisha kituo kitakachoendeshwa na watu wenye ujuzi.

Collins anafanya kazi na vijana wa rika lake, ana hamu ya kujifunza mengi kutoka kwa vijana wenzake na wakati huo huo anawatia moyo wa kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha malengo yao. Ephantus Kamau anafanya kazi pia katika Slum TV. Yeye huenda katika eneo la mabanda la Mathare kutafuta habari na kupiga filamu za video. Yeye ndie naibu mratibu wa Slum TV.

**16. Soundbyte Ephantus Kamau 1 (English)**

*"Aaa kuishi kwenye maeneo ya mabanda –maisha yanaweza kuwa mabaya kweli, lakini kuna taarifa za mafanikio pia, kuna vipaji vingi ambavyo havitambuliwi ulimwenguni. Nia hasa ya mimi kujiunga na hii Slum TV, ni kwa sababu nilitaka nipate fursa ya kuueleza ulimwengu kuwa inawezekana kupata mambo mazuri kutoka katika sehemu za mabanda."*

**17. SFX Screening of Slum TV production**

**18. Narrator**

Siku ya maonyesho imewadia! Ni mwendo wa saa 12 jioni, ni wakati wa machweo ya jua. Leo hii Ephantus na Collins wametambua kuwa kazi yao imezaa matunda. Zaidi ya watu 2000 wamekusanyika katika uwanja wa Mathare kwa ajili ya kutazama filamu mpya walizotayarisha. Marika yote yamekusanyika hapo, kina mama na watoto wao migongoni, wazee na fimbo zao za mikononi pamoja na watoto, wote hawa wamefika. Filamu zitakazoonyeshwa leo ni kuhusu "Watu Maalum" – ni kuhusu

dereva bora wa matatu au dalala, na mnoaji visu hodari. Ephantus anafurahia kila dakika ya onyesho hilo.

**19. Soundbyte Ephantus Kamau 2 (English)**

*“Wow! Vizuri sana. Siku kama hii sote huwa tunaisubiri kwa hamu kwa sababu tukianza tu kucheza muziki kabla ya kuanza kuonyesha filamu, kila mtu huwa anakuja kuangalia tunataka kufanya nini. Kwa hivyo huwa tunapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa jamii. Jamii inatupenda sana, watu wetu wanapendezwa na kazi tunayoifanya. Kila mara tunapofanya maonyesho watu huwa wanatuuliza juu ya onyesho litakalofuata.”*

**20. SFX Machine sound in the slum**

**21. Narrator**

Baadhi ya watu katika jamii ya Mathare hawaipendi Slum TV – na mara nyingine inakuwa hatari kupiga picha za video. Kwa mfano watengenezaji wa pombe haramu hawapendi kuona kamera karibu yao. Lakini hawana jinsi ya kumzuia Collins kufanya kazi yake.

**22. Soundbyte Collins Omondi 5 (English)**

*“Mimi siogopi, kwa sababu hiyo ni kawaida, Mimi ni shujaa. Ni jambo la kuzungumza nao tu, na kwa sasa tuna maafisa wa usalama katika Slum TV. Wao ndio wanatusaidia tuweze kuwafikia hao wanaotengeneza pombe.”*

**23. Narrator**

Kazi yake imemfanya Collins Omondi kuwa mtu maarufu miongoni mwa vijana, kote katika eneo la mabanda la Mathare na nje ya eneo hilo. Billian Okoth ni mwanamuziki kutoka mtaa wa Eastleigh unaopakana na

eneo la Mathare. Anashirikiana kwa karibu na Slum TV, yeye ni kati ya wanamuziki wanaotumbuiza kila wakati kabla maonyesho ya filamu kuanza.

**24. Soundbyte Billian Okoth 1 (English)**

*"Ni kweli Collins ni rafiki mwema. Yeye hutabasamu wakati wote, kila ninapomuona na kamera mimi hujisemea kuwa atafika mbali sana, amini usiamini atafika mbali kwa sababu anajitolea sana kwenye kazi yake, kila wakati anatafuta ushauri, anafanya jitihada kwa kila kitu. Nimemjua kutokana na Slum TV na pia kutokana na kazi yake. Kipaji chake na ujuzi anaopata kutoka kwenye Slum TV najua utamfikisha mbali. Yeye ni mtu mzuri sana."*

**25. Narrator**

Collins Omondi amefanya bidii kubwa, anaweza kabisa kufika mbali japo kuwa anakabiliwa na ushindani mkubwa. Muhimu ni kwamba leo analeta mabadiliko kwa jamii ya Mathare, huenda kesho akaleta mabadiliko kwa Wakenya wote!

**OUTRO (Announcer):**

Ni hayo tu kwa leo katika makala ya Noa Bongo jenga Maisha Yako, kipindi cha leo kimeandikwa na Josephat Charo. Kumbuka kuwa unaweza kujifunza mengi kuhusu kipindi hiki au pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe
Asante kwa kutusikiliza na hadi wakati mwingine, Kwaheri!

**END**